



SYRACUSE CITY SCHOOL DISTRICT

Jaime Alicea, Msimamizi wa Shule

Ofisi ya Msimamizi

Jumanne, 31 Machi 2020

Kwa Familia za Syracuse City School District,

Tarehe 27 Machi Gavana Cuomo alitangaza kuwa shule zote katika Jimbo la New York zitafungwa hadi tarehe 15. Tumekuwa tukishirikiana na Idara ya Elimu ya Jimbo la New York (New York State Education Department) na Ofisi ya Gavana tangu tangazo hilo ili kuthibitisha jinsi uamuzi huu utakavyoathiri Mapumziko yetu ya Aprili tuliyoratibu awali (6-10 Aprili)

Sasa tunajua kuwa lazima wilaya zote ziendelee kutoa mafunzo ya mbali kwa wanafunzi, milo ya wanafunzi na huduma ya watoto kwa wafanyakazi msingi kila siku ya juma kati ya tarehe 1 Aprili, 2020 na tarehe 14 Aprili, 2020 hata kama wilaya itaratibiwa kuwa kwenye mapumziko ya majira ya kuchipua kipindi hicho. Hii inamaanisha kuwa tutaendelea kutoa usaidizi wa elimu na milo kwa wanafunzi wetu wakati wa Mapumziko yetu ya Aprili tuliyoidhinisha na kuratibu awali.

Walimu, wasimamizi na wafanyakazi wataendelea kutoa huduma ya elimu kwa wanafunzi wote wiki ya tarehe 6-10 Aprili. Ni tumaini letu kuwa utadumisha ratiba sawa na mtoto wako na kuendelea kumhimiza kukamilisha kazi waliyopewa. Pia tutaoa huduma za stafthai na chamcha za grab and go kwenye maeneo yetu tuliyoteua kuanzia saa 10:00 asubuhi hadi saa 12:00 adhuhuri Jumatatu, Jumatano na Ijumaa.

Kutokana na shule kufungwa, tumbaini kuwa tarehe 6 Machi, 2020, sasa itakuwa tarehe ya mwisho ya kipindi cha usahihishaji wa tatu. Wanafunzi watakuwa na hadi tarehe 10 Aprili kuwasilisha kazi yoyote waliyopewa kabla ya tarehe 6 Machi. Ikiwa mtoto wako ana swali lolote kuhusu mazoezi yoyote kutoka kwenye kipindi cha usahihishaji wa tatu tafadhali mshauri awasiliane na mwalimu wake au mkuu wao wa jengo.

Ningependa kuwashukuru kwa usaidizi na uvumilivu wenu tunaposhirikiana katika kipindi hiki cha wakati ambao haujawahi kutokea.

Tafadhali endelea kuwa salama,

A handwritten signature in black ink that reads "Jaime Alicea".

Jaime Alicea
Msimamizi wa Shule